

Fasiri

Mwongozo wa Tafiti za Utabibu wa Virusi Vya UKIMWI kwa ajili ya Bodi ya Ushauri ya Jamii (CAB).

IMPAACT
International Maternal Pediatric Adolescent AIDS Clinical Trials Group

François-Xavier Bagnoud Center
University of Medicine & Dentistry of New Jersey

Fasiri hii imetayarishwa kwa dhamira ya kuwasaidia washirika wa Bodi ya Ushauri ya jamii (CAB) chini ya IMPAACT katika kazi zao. Maneno yanayotafsiriwa hapa na vifupisho vilivyomo vinajumuisha yale yanayotumika zaidi katika mitandao ya tafiti na katika protokali za majaribio. Maneno mengi katika fasiri hii yametafsiriwa hapa kwa sababu yameainishwa katika mwongozo wa mafunzo kwa ajili ya Bodi za Ushauri za Jamii chini ya IMPAACT.

Vifungu na vifupisho vimeorodheshwa kwa mpangilio wa kialfabeti. Maneno mengine yaliyotumika katika vifungu yameandikwa kwa italicized. Maneno yanoonekana kwa herufi za italics inaashiria kwamba yanatumika neno hilo limetafsiriwa tena sehemu nyingine katika kamusi hii.

Zana hii iliandaliwa na 'the François-Xavier Bagnoud Center katika University of Medicine and Dentistry of New Jersey (UMDNJ)',kwa na msaada wa 'the International Maternal Pediatric Adolescent AIDS Clinical Trials Group (IMPAACT)'. Vyanzo vya baadhi ya tafsiri imeambatanishwa mwishoni mwa kijitabu hiki.

Dondoo kutoka machapisho haya yanaweza kufanyiwa nakala bila kizuizi ama pia kutoholewa kwa kutambua chimbuko lake, ili mradi machapisho hayo ni kwa ajili ya kufanyia mafunzo yasiyo ya kutengeneza faida tu. Taadhali peleka maoni ama masuali kwa info@fxbcenter.org

IMPAACT
International Maternal Pediatric Adolescent AIDS Clinical Trials Group

François-Xavier Bagnoud Center
University of Medicine & Dentistry of New Jersey

Orodha ya yaliyomo

Orodha ya yaliyomo

A 5
B 5
C 7
D 7
E.....8
F.....8
H 8
I.....9
J.....9
K.....10
L.....14
M.....14
N 17
P.....17
R 18
S.....18
T.....19
U 20
V.....23
W.....23
Y.....24
Z.....24

Fasihi vifupisho (akronimi)

A 25
B 25
C 25
D 26
E.....26
F.....26
G 26
H 26
I.....27
K.....27
L.....27
M.....27
N 28
O 28
P.....28
Q 29
R 29
S.....29
T.....29
U 29
V.....30
W.....30
X.....30
Z.....30

Fasiri

ya maneno yanayotumika kwa kawaida katika tafiti za kitabibu za Virusi Vya UKIMWI

A

Adilifu: Ya haki, sahihi, au ya usawa

Afua: Kitendo kinachofanyika ili kubadilisha jambo linalotokea ama linaloweza kutokea, haswa kwa kuzia kitu ambacho sio kzuzi. Kwa mfano, kufundisha zile ABCs za kuzuia uambukizo wa VVU ni afua iliyoandaliwa ili kupunguza hatari ya uambukizaji wa VVU.

Anayejidunga dawa (Teja): Mtu amayejidunga dawa kwa misingi isiyo ya ki-tiba

Antijeni: Ni chochote ambacho kinaweza kusisimua mwili ili uweze kuzalisha kingamwili (Mtano: VVU vinaweza kuwa antijeni).

Asasi za Kijamii(AZAKI): Shirika la huduma ndani ya jamii.Kwa mfano, shirika lisilo la kutengeneza faida linalotoa huduma ya unasihi na huduma nyingine za kijamii kwa watu wenye VVU katika eneo maalumu la jamii ni AZAKI.

Asilimia ya chembechembe za CD4: Ni asilimia ya chembechembe nyeupe za damu katika kingamaradhi ambazo ni chembechembe za CD4. Asilimia ya chembechembe za CD4 ni kiashiria halisi zaidi kwa hali ya kingamaradhi kuliko idadi ya chembechembe za CD4.

Athari (Angalia athari kinzani): Athari za dawa ambazo hazikutarajiwa

Athari mbaya (AE) (pia yajulikana kama athari ama madhara yasiyofaa): Dalili isiyofaa ama tatizo la kitabibu lililosababishwa na dawa.

Awamu ya I ya jaribio: Kujaribisha dawa kwa kuangalia usalama na kipimo chake katika idadi ndogo ya watu wenye afya; mfano (watu 10 hadi 100)

Awamu ya II jaribio: Kujaribisha dawa kwa kuangalia usalama kwa kundi kubwa zaidi la watu (50 hadi 500) wenye ugonjwa au dalili za ugonjwa ambao dawa hiyo inadhamiriwa kutibu.

Awamu ya III jaribio: Kujaribisha dawa kwa kundi kubwa la watu (mamia ama maelfu) wenye ugonjwa au dalili za ugonjwa ambao dawa hiyo inadhamiriwa kutibu, ili kukung'amua kama dawa hiyo inao uwezo na ni salama.

Awamu ya IV ya jaribio: Jaribio la kitabibu hufanyika baada ya dawa kuidhinishwa na kuruhusiwa. Jaribio la awamu ya IV hung'amua usalama na uwezo wa tiba iliyoidhinishwa katika kipindi cha muda mrefu. Wakati awamu III za majaribio hazichukui zaidi ya miaka 2 hadi 3, Awamu ya IV ya jaribio huweza kuendeshwa kwa miaka 5-10 ama zaidi.

Awamu: Hatua za majaribio ya kitabibu

B

Badiliko la Kipooza-uongo: Badiliko la kuonekana ama la ki-hisia, linalotokea baada ya kiini fulani kutumika, ambacho sio matokeo ya kitu chochote mahususi cha kiini hicho. Badiliko hili laweza kuwa la faida ikionesha matarajio ya mshiriki na, mara nyingi, ni matarajio ya mtu yule ambaye anatoa kiini hicho.

Badiliko: Ni badliko linalopatikana katika VVU linaloweza kurithishwa kwenye nakala nyingine za VVU. Iwapo nakala hizo (zinazotengeneza virusi vipya) hazitathibitiwa vyema (virusi huwa na nguvu na wingi wa idadi ya virusi inakuwa kubwa), badiliko linaweza kutokea ili VVU viweze kubadilika na kuwa sugu kwa dawa za kupambana na VVU.

Bila jina: Isiyo na jina ama utambulisho

Bila mpangilio madhubuti (Randomization): Upangiliaji kwa kutumia komputa kwa njia ya kubahatisha kwa hilo kundi la majaribio (la utafiti) au lile kundi la kudhibiti/kulinganisha (la kiwango cha msaada au la kipooza-uongo).

Bila Tiba (Treatment naïve): Ni mtu ambaye hajawahi kutumia dawa dhidi ya VVU

Bila-kufumbwa/Iliyo wazi: Washiriki na/au pamoja na watafiti hupewa taarifa kuhusu tiba mahususi wanayopatiwa washiriki ambao hapo awali walikuwa wamefumbwa "kufumbwa" (hawakujulikana)

Bodi ya Ki-taasisi ya Mapitio (Institutional Review Board-IRB) (Tazama Kamati ya maadili): Ni Kamati ya watu ambao ni lazima watoe kibali kabla utafiti wa kitabibu haujaruhusiwa kuanza. Kila kitengo cha jaribio la kitabibu ni lazima kipate idhini kutoka Kamati ya Maadili (ama IRB). Kamati hii pia hufuatilia tafiti hizi wakati zikiendelea ili kutazama mambo ya kiusalama yasiyotarajiwa, mambo yanayohusiana na haki za washiriki, na kuhusiana na tabia za kimaadili za kila mtafiti na timu nzima ya watafiti.

Bodi ya Usalama na Ufuatiliaji (DSMB): Ni kamati huru inayoundwa na wataalamu wa utafiti wa kitibabu. Wanajadili taarifa wakati utafiti unaendelea, ili kuona kunakuwepo hatari za kiusalama na kuona kama malengo ya jaribio yamefikiwa. DSMB inaweza kupendekeza kuwa dawa ya jaribio isitishwe iwapo kuna hatari za kiusafalama au kama dawa ya uchunguzi inathibitishwa kuwa na manufaa zaidi kuliko ile tiba ya kiwango.

Bodi ya Ushauri ya jamii ya IMPAACT (IMPAACT Community Advisory Board (ICAB): Kikundi cha kimataifa cha wawakilishi wa jamii inayojumuisha viongozi kutoka katika wajumbe wa Bodi za ushauri za jamii za maeneo yao na ya kikanda (CABs)

Bodi ya ushauri ya jamii ya Mtandao wa Mshikamano/mtambuka (Cross network CAB): Angalia wadau wa jamii

Bodi ya ushauri ya jamii(CAB): CAB ni kikundi cha watu wanaowakilisha jamii pale ambapo utafiti unafanyika. Wajumbe wa CAB wanao wajibu wa tutia moyo mawasiliano kati ya jamii na watafiti wa kisayansi. Wajumbe wa CAB huelimisha jamii kuhusu utafiti kwa ujumla na kuhusu jaribio maalumu la kitabibu lililobuniwa ama linalotekelezwa katika mtandao. Wajumbe wa CAB huwataarifu watafiti kuhusu mahitaji ya jamii na shauku za jamii, na wanatoa mrejesho kwa watafiti kutoka kwa jamii kuhusu masuala yanayohusiana na mipango ya mitandao ya utafiti.

Bodi ya Ushauri ya Kanda (Regional Community Advisory Board -RCAB): Ni kamati ya wawakilishi kutoka bodi za washauri katika kanda moja ya kigeographia (kama vile Afrika kusini mwa-Sahara au Marekani ya magharibi), wanaokutana kuzungumzia masuala ya jamii yanayohusiana na utafiti na VVU yaliyo ya kawaida miongoni mwa vituo vyao vya utafiti – CTUs katika kanda.

C

Chambua: Kuchanganua takwimu (taarifa) ili kubaini matokea ya jaribio la kitabibu.

Chanjo ya ahueni ya VVU (Therapeutic HIV vaccine): Ni chanjo ya VVU inayotumika kumtibu mtu mwenye uambukizo wa VVU. Chanjo ya ahueni ya VVU hutengenezwa ili kuimarisha mwitikio mzuri wa kingamwili dhidi ya uambukizo wa VVU, ili kuzuia vizuri zaidi virusi.

Chanjo ya kuzuia VVU: Ni chanjo inayolenga kuzuia uambukizo wa VVU kwa watu ambao hawajaambukizwa.

Chanjo: Ni kiini ambacho husisimua mwitikio wa kinga-mwili ili kuzuia au kudhibiti uambukizo. Chanjo kwa kawaida hutengenezwa kutokana na sehemu za bacteria au kirusi ambacho peke yake hakiwezi kusababaisha uambukizo. Watafiti hujaribisha chanjo kwa ajili ya kuzuia na kutibu VVU.

Chembe-chembe za aina ya T (pia hujulikana kama Chembechembe za CD4 au limphosaiti za CD4): Ni aina ya Chembechembe nyeupe za damu katika kinga-mwili zinazosaidia kuukinga mwili kutokana na uambukizo. Uharibifu wa chembechembe za CD4 kutokana na VVU huathiri kingamwili, humwacha mtu katika hatari kubwa zaidi ya uambukizo mkubwa au maradhi.

Chembechembe za CD4 (pia zajulikana kama chembechembe za T): Ni aina ya chembechembe nyeupe za damu za aina ya A katika kinga ya mwili ambazo zinasadia kuukinga mwili kutokana na uambukizo. VVU vinaharibu chembechembe za CD4, kuharibu kinga-mwili na kumwacha mtu katika hali hatarishi zaidi ya uambukizo au maradhi.

Chembechembe za CD8: Ni aina ya chembechembe nyeupe za damu katika kingamaradhi ambazo zinazuia kuzalisha kingamwili na miitikio mingine ya kingamaradhi.

D

Dalili za kurudisha tena kingamwili (Immune reconstitution syndrome -IRS): (Pia hujulikana kama kurudisha tena kingamwili (IRD) au dalili za kuunda tena kingamwili [IRIS]): Athari za aina ya uvimbe zinaweza kutokea pale ambapo kingamwili ya mtu inaboreshwa baada ya kuwa mdhaifu sana, kama vile mtu mwenye UKIMWI anapoanza kutumia dawa dhidi ya VVU na anapata ongezeko la haraka katika wingi wa chembe-chembe za CD4. Homa, pamoja na kuvimba, wekundu, ama usaha sehemu iliyoumia ama uambukizo vinaweza kuashiria kwamba uambukizo ambao hapo awali haukutambulika kwa udhaifu wa kingamwili sasa unashambuliwa na kingamwili yenye nguvu zaidi. Ijapokuwa hii inaashiria kwamba kingamwili ya mtu huyu inaimarika kiafya, inaweza kuwa mbaya, mara nyingine kusababisha hali ya kifo na nilazima ipatiwe tiba. IRS haiashirii kushindwa kwa tiba dhidi ya VVU.

Dalili: Ni dalili za ujumla au hali zinazotokea kwa pamoja na kuashiria ugonjwa fulani au mianya inayoongeza uwezekano wa kuanza kwa ugonjwa.

Dawa mpya ya majaribio (IND): Ni dawa inayofanyiwa majaribio katika jaribio la kitabibu

Dawa ya uchunguzi/dawa: Ni dawa ambayo haijaidhinishwa wala kupata leseni ya kutumika kwa binadamu

Dawa za kupunguza makali ya VVU (ARV): Ni dawa dhidi ya VVU (Tazama Tiba ya dawa za kupunguza makali ya VVU)

Dawa: Katika nyanja za matibabu, dawa ni mchanganyiko wa dawa zilizoainishwa kutibu hali au ugonjwa

Dhahiri: Iliyohakikishwa. Kufuatana na takwimu za jaribio, na sio kwa nadharia

Division of Acquired Immunodeficiency Syndrome (DAIDS): Ni kitengo kinachofadhiliwa na serikali ya Marekani chini ya National Institute of Allergy and Infectious Disease. DAIDS inianzishwa mwaka 1986 ili kufuatilia mahitaji ya kitafiti yanayohusiana na uambukizo wa VVU.

Dozi-mchanganyiko (FDC): Ni kidonge chenye dozi ya mchanganyiko wa dozi ya dawa mbili au zaidi

E

ELISA/Western Blot (Tazama jaribio la kinga-maradhi za VVU): Upimaji wa damu ili kugundua kuwepo au kutokuwepo kwa kingamwili za VVU katika damu

Enye-kuharibika kwa urahisi: Katika mukhutadha ya VVU, dhana hii hututumika kuelezea aina ya VVU ambayo sio sugu kwa dawa yoyote maalumu dhidi ya VVU. Hutumika pia kuelezea kuwepo kwa hali ndogo sana ya usugu katika magonjwa mahsusi ya kuambukizwa.

F

Ficho-Isiyo na dalili: Isiyo na dalili au dalili za ugonjwa.

Fomu ya Muhtasari wa Fikra/wazo(CS): Maelezo ya kifupi kuhusu pendekezo la jaribio la uchunguzi ama jaribio la kitabibu

Fomu ya ridhaa: Ni fomu inayotoa maelezo yaliyoandikwa kwa kina kuhusu jaribio la kitabibu. Kwa kuweka saini katika fomu ya ridhaa inaashiria kwamba mtu huyo ameelewa taarifa aliyoipata, na kwa hiari anajisajili katika jaribio. Fomu hii sio sawa na kutia saini mkataba, kwa sababu mshiriki anaweza kuamua kusitisha kushiriki katika jaribio wakati wowote (kujitoa katika jaribio).

Fomu ya Uchambuzi wa Muhtasari wa Fikra (DACS): Andiko la kuchambua taarifa kutoka katika protokali zinazoendelea ili kuelezea suali mahususi la kisayansi

Fomu za kisa mkasa (CRF): Fomu zinazotumika kukusanya takwimu za jaribio la kitabibu.

H

Haki: Kufanya sawa

Halali: Kuthaminisha bila upendeleo

Hali tata: Matatizo yatokanayo na ugonjwa ama tiba yake.

Hali ya kufadhaisha: Sifa yoyote zaidi ya ile tiba ambayo inaweza kuleta athari katika majaribio ya kitabibu

Hatari: Uwezekano wa kupata madhara ama kupoteza; hatari

Hatarini-kwa VVU: Wakati mtu amapokuwa katika mazingira ya VVU kwa njia ambayo ina uwezekanano wa uambukizo wa kirusi kwa mtu huyo. Kwa mfano, watoto wachanga wa wamama mwenye uambukizo wa VVU wapo hatarini wakati wa ujauzito, uchungu na kujifungua, na wakati wa unyonyeshaji, hivyo watoto wachanga wako hatarini-kwa VVU na hivyo katika hatari ya kupata uambukizo wa VVU.

Hatua za Tanner (Tanner staging): Ni njia ya kimpangilio ya kutambua hatua ya balehe kwa kijana. Katika tiba ya VVU, Hatua za Tanner hutumika kutambua miongozo muafaka ya tiba ya kufuata (kwa watu wazima, vijana, au watoto).

Hesabu ya vidonge: Ni njia ya kupima namna ya ufuasi wa dawa za kupunguza makali ya VVU (ART) ambayo inahusisha kuhesabu idadi ya vidonge vinavyomezwa ikilinganishwa na idadi ya vidonge vilivyostahili kumezwa iwapo mgonjwa angezingatia kiwango cha dawa alizoandikiwa katika tiba.

Hiari: Inatikana na uchaguzi wa mtu badala ya shinikizo kutoka kwa wengine.

Highly Active Antiretroviral Therapy (HAART): Tiba ya uambukizo wa VVU kwa kutumia mchanganyiko wa dawa za kupunguza makali ya VVU (ARV) kutokana na angalau makundi mawili

HIV RNA PCR (pia hujulikana kama wingi/mzigo wa virusi): Kipimo cha damu kinachopima kiasi cha VVU katika damu ya mtu mwenye uambukizo. Kupima wingi wa virusi ni njia mojawapo ya kunga'mua ni kwa kiasi gani dawa za kupunguza makali ya VVU (ARVs) zinafanya kazi. Dawa za kupunguza makali ya VVU (ARV) za manufaa zinaweza kupunguza wingi wa VVU hadi kiwango ambacho kinaweza kupimika katika maabara (kiwango kisichoonekana). Iwapo wingi wa VVU utaongezeka wakati dawa za kupunguza makali ya VVU (ARV) zinatumika, inaweza kuashiria kwamba kwamba dawa si ya manufaa ama haitumiki kwa usahihi.

Huduma ya tiba iliyowekewa kigezo kwenye kinga-mwili (Immune-based therapy - IBT): Huduma ya kuleta ahueni inayotumia mrengo unaolenga kuimarisha kingamwili ili kukabiliana na uambukizo wa VVU

I

Idadi ya chembechembe za CD4: Ni njia mbadala ya kupima ni kwa kiasi gani madhara yamekwisha kufanywa na VVU katika kinga-mwili.

Idadi ya watu: Kundi la watu wa ujirani, mji, mkoa, nchi, au thamani moja. Katika utafiti, idadi ya watu inayotakiwa kufanywa uchunguzi katika jaribio la kitabibu ni kundi la watu ambao wana thamani mahususi za afya (kama uambukizo wa VVU).

International Maternal Pediatric Adolescent AIDS Clinical Trials Group (IMPAACT): Ni mtandao unaofadhiliwa na DAIDS. Utume wa IMPAACT ni kushusha kwa kiwango kikubwa uwezekano wa vifo na ugonjwa unaohusiana na VVU miongoni mwa wanawake wajawazito, watoto na vijana.

Intrapartum: Ni kipindi kati ya uchungu na kujifungua

Isiyo-elekevu (Non-directive): Kutoa habari kamili na sahihi bila kujaribu kushawishi muamuzi ya mtu

Isiyofungamana (Neutral): Tazama isiyo-elekevu (Non-directive).

J

Jamii: Kundi la watu wenye jambo linalowahusu kwa pamoja, wanaoishi katika eneo moja maalumu ama kuhusiana.

Jaribio chini ya uangalizi: Ni jaribio la kitabibu ambalo halitoi tiba ya uchunguzi. Washiriki huchunguzwa na takwimu za afya huchukuliwa na kuwekwa kwenye kumbukumbu kwa kipindi cha muda fulani.

Jaribio la kitabibu la kutokuwa na mpangilio madhubuti: Ni jaribio ambamo washiriki wanapatiwa usajili katika mkondo mmoja miongoni mwa mikondo miwili au

zaidi ya matibabu bila mpangilio katika jaribio hilo la kitabibu.

Jaribio la kitabibu linalothibitiwa: Ni jaribio la kitabibu ambamo kundi moja la washiriki linapewa dawa za majaribio (kundi la kuchunguzwa) na hulinganishwa na kundi la washiriki wanaotumia tiba ya kiwango (kundi kithibiti).

Jaribio la upofu-mara mbili: Ni aina ya jaribio ambamo si mshiriki wala mtafiti anayejua ni tiba ipi mshiriki anapewa

Jaribio la vipimo-vingi: Ni jaribio la kitabibu ambamo vipimo zaidi ya kimoja katika aina hiyo-hiyo ya dawa hujaribiwa samambamba na nyingine ili kung'amua ni kipimo kipi kinafanya kazi vizuri zaidi na chenye madhara kidogo kabisa

Jaribio la wazi: Halikufungwa. Mtafiti na washiriki wanajua ni dawa ipi mshiriki anapatiwa.

Jaribio lenye kuthibitiwa na Kipooza-uongo: Ni jaribio ambalo kundi la ulinganishi hupewa Kipooza-uongo. Tazama Kipooza-uongo.

Jaribio lililofumbwa au iliyofumbwa zaidi: Si mshiriki wala mtafiti anayejua ni mkondo upi mshiriki amepangwa.

Jaribio linganishi: Katika majaribio linganishi ya kitabibu, kundi moja la washiriki wanapokea ile dawa ya majaribio huku kundi lingine la washiriki wanapokea tiba ile ya kiwango. "Tiba ya Kiwango" inamaanisha ile dawa ambayo kwa kawaida hutolewa kwa watu ambao hawashiriki katika jaribio kama tiba ya matatizo ya kiafya yanayofanyiwa uchunguzi. Lile kundi la washiriki ambao wanapatiwa tiba ya kiwango hujulikana kama "kundi kidhibiti".

Jumla: Mjumuisho wa kitu ama nyongeza katika idadi ya washiriki kwenye jaribio la kitabibu.

K

Kabla ya kuzaa (kabla ya Kuzaa): Kabla ya kuzaa

Kamati Tendaji ya Mtandao (Network Executive Committee - NEC): Kundi la watafiti ambao wanawakilisha uongozi wa mtandao wa utafiti na kusimamia agenda za kisayansi na utekelezaji wake.

Kamati ya Kutathmini Utendaji na Nguvu Kazi (Performance Evaluation Resource Committee - PERC): Ni kamati ya IMPAACT inayowajibika na uangalizi ya matendo ya kila mtu katika kila kituo cha utafiti wa kitabibu (CTUs)

Kamati ya Maadili (Tazama Institutional Review Board or IRB): Ni Kamati ya watu wanaotoa kibali kabla utafiti wa kitabibu haujaruhusiwa kuanza. Kila kitengo cha jaribio la kitabibu ni lazima kipate idhini kutoka Kamati ya Maadili (ama IRB). Kamati hii pia hufuatilia tafiti hizi wakati zikiendelea ili kutazama mambo ya kiusalama yasiyotarajiwa, mambo yanayohusiana na haki za washiriki, na kuhusiana na tabia za kimaadili za kila mtafiti na timu nzima ya watafiti.

Kamati ya Uangalizi wa kisayansi (Scientific Oversight Committee-SOC): Kamati ya uongozi ya mtandao wa majaribio ya kitabibu ya IMPAACT husimamia agenda za kisayansi za mtandao huo.

Katika mishipa: Kupiga sindano moja kwa moja katika mishipa

Kigezo cha kujumuishwa: Kigezo cha kiafya ama kijamii cha kiwango fulani amabacho hutumika kuainisha iwapo mtu anaweza kuruhusiwa kujiunga na jaribio la kitabibu.

Kigezo cha kutoshiriki: Ni sifa zinazomfanya mshiriki kutokubalika kwa mtu anayejitolea kusajilwa katika jaribio fulani

Kigezo cha ustahiki (Tazama vigezo vya kujumuishwa na kutokujumuishwa): Ni sifa za ujumla zinazohitajika ili kujiunga na jaribio la kitabibu(kama vile umri au jinsia) na tabia mahsusi (kama vile wingi au uchache wa virusi au matibabu ya awali ya VVU)

Kigezo: Kiwango ambacho kwacho mambo huchukuliwa maamuzi. Kwa mfano, kigezo kimojawapo kinachotumika kupima mafanikio ya tiba ya VVU ni wingi ama uchache wa VVU.

Kikundi (pia hujulikana kama kundi la jaribio): Katika muktadha ya jaribio la kitabibu, kundi la jaribio ni lile kundi la washiriki ambao ni miongoni mwa ile idadi ya watu wanaofanyiwa jaribio.

Kinga: Kitu kinachozuia ana kukinga tukio au shughuli

Kinga: Kizuizi dhidi ya….. ama kukinga dhidi ya ugonjwa

Kinga—mwili iliyo—kandamizwa (Immunosuppressed): (Angalia Kinga isiyo na uwezo wa kutoa mwitikio—Immunocompromised)

Kingamwili-antibodi: Protini inayozalishwa na mfumo wa mwili wa kukinga maradhi ambayo inatambua na kupigana na chembechembe za uambukizo zinazoingia mwilini. Kila kingamwili ni maalumu kwa aina maalumu ya chembechembe ya uambukizo (kwa mfano kingamwili za VVU ama kingamwili za surua).

Kinga-uwezo (Immunocompetent): Kuweza kuhimili mwitikio wa kinga wa kawaida kukabiliana na virusi ama bakteria

Kipau-mbele: Kuagiza vitu kulingana na umuhimu wake

Kipimo cha haraka (Rapid test): Ni aina ya kipimo cha kugundua kinga-maradhi dhidi ya VVU ndani ya damu ndani ya kipindi chini ya dakika 30 na kikawa na usahihi wa asilimia 99%.

Kipimo cha kingamaradhi: (Tazama ELISA/Western Blot): Kipimo cha damu kinachotumika kutambua kuwepo ama kutokuwepo kwa kingamaradhi za VVU katika damu. Kipimo kinachoonesha kuwepo kwa mtu wa umri wa miezi 18 na zaidi inaashiria kwamba mtu huyo ana uambukizo wa VVU.

Kipimo cha usugu: Kipimo cha maabara kung'amua uwapo wa dalili za usugu kwa mtu huyo kwa dawa yoyote dhidi ya VVU.

Kipindi cha maatamizi (Sero-conversion): Ni mchakato ambamo mtu ambaye amepata uambukizo mpya wa VVU huanza kutengeneza kinga-maradhi za VVU.

Kipindi cha mficho: Ni kile kipindi cha muda kati ya mtu anapopata uambukizo VVU kwa mara ya kwanza na pale ambapo zitajitokeza kinga-maradhi zinazoweza kuonekana. Kwa sababu kinga-maradhi za VVU huchukua muda kujitengeneza, kipimo cha kinga-maradhi ya VVU hakitaonesha kuwepo kwa VVU baada tu ya mtu kupata uambukizo. Kipindi hiki kwa kawaida huwa kati ya siku 14 hadi 21, lakini hutofautiana. Karibu kila aliyeambukizwa VVU atakuwa na kinga-maradhi zinazoonekana kwenye kipindi katika kipindi cha miezi 3 baada ya uambukizo.

Kipooza-uongo (Placebo): Ni kidonge kinachofanana na dawa ya majaribio lakini hakina dawa ndani yake.

Kisa: Ni taarifa/mkasa unaoelekeza kitu ambacho si cha kawaida ambacho kimetokea kwa mgonjwa huyo. Kisa mkasa kinawawezesha madaktari kuainisha VVU na baadaye, UKIMWI.

Kisaidizi: Kiini kinachoongezwa katika dawa kinachoboresha ile dawa asilia. Kwa mfano, kuongeza aspirini ama acetaminophen katika dawa ya kupunguza maumivu aina ya narcotic ili kuongezea nguvu uwezo wa dawa hiyo ya narcotic kwa kupunguza maumivu. Kisaidizi kinamaanisha pia kiini kinachoongezwa katika chanjo ili kuboresha uwezo wa kinga za mwili kuendana na chanjo yenyewe.

Kisasili (Imani potofu): Imani ya kawaida ama mila iliyoenea kuhusu kitu Fulani ama mtu Fulani.

Kitengo cha majaribio ya kitabibu (CTU): Eneo ambalo ni sehemu ya mtandao wa utafiti wa kitabibu. CTU hutekeleza jaribio la kitabibu, na huchangia utaalamu wa kuandaa utafiti kwa ushirikiano na wataalamu wengine ndani ya huo mtandao.

Kituo cha François-Xavier Bagnoud (FXB): FXB wanatoa huduma ya matunzo ya kitabibu, elimu, na misaada ya kiufundi ndani ya Marekani na kimataifa kuunga mkono kujenga uwezo kwa ajili ya kujihusisha na janga la UKIMWI. FXB huongoza programu za mafunzo ya tafiti za kitabibu kwa vituo vya kimataifa vya CTU vinavyohusiana na PACTG na IMPACT.

Kituo cha kuhifadhi takwimu (DMC): Ni kituo cha kiutawala kinachounga mkono ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu kutoka katika majaribio ya kitabibu. Kituo cha kuhifadhi takwimu cha IMPAACT kinajulikana kama Frontier Science and Technology Research Foundation (FSTRF)

Kituo cha Kuzuia maradhi (CDC): Ni wakala ya Kimarekani yenye jukumu la kusukuma mbele masuala ya afya kwa kuzuia na kudhibiti maradhi, majeraha na, ulemavu.

Kituo cha utendaji (Operations Center - OPS Center): Ni kitengo cha utawala kwa ajili ya mtandao wa utafiti wa kitabibu, ambapo wafanyakazi wake wanawajibika kwa kuratibu, kusimamia, kufuatilia, kuchukua taarifa, na kutoa msaada kwa shughuli zote za huo mtandao wa utafiti.

Kiwango (Rate): Kiwango cha badiliko ikilinganishwa na takwimu za msingi. Kwa mfano, kiwango cha kushindwa kwa vairologia ndani ya kundi lile la majaribio ikilinganishwa na kiwango cha kushindwa kwa vairologia katika kundi lile la uthibiti baada ya majuma 24 ya tiba

Kiwango cha hatari-faida: Ni ile dhana ya kufikiria hatari kwa mshiriki mmojawapo katika jaribio la kitabibu kulinganisha na faida zinazotarajiwa

Kiwango cha kuenea: Ni sehemu miongoni mwa ile idadi ya watu waliyokumbwa na ugonjwa katika muda mfupi kama vile kupiga picha ya haraka, mfano; mwaka 2003, asilimia 25% ya watu wazima katika nchi ya Y walikuwa na uambukizo wa VVU.

Kuchuja/Uchujaji: Ni vipimo na uchunguzi unaohitajika ili kuhakiki kama mtu huyu anayejitolea ana sifa za kushiriki katika jaribio hilo la kitabibu. Kuhakiki iwapo mtu huyu anayejitolea anafikia vigezo vinavyohitajika na jaribio.

Kufa: Kifo

Kufaa: Yenye kuleta matokeo ya kufaa katika kutibu ama kukinga tatizo la kitiba

Kuitathmini jamii: Kuainisha kiwango cha sasa cha uelewa na mahitaji ya mafunzo kwa jamii husika

Kujiandikisha zaidi ya mara moja: Kushiriki katika jaribio zaidi ya moja kwa wakati huo huo.

Kujitoa: Kukataa kuendelea au kukataa tiba

Kundi (la dawa): Ni kundi la dawa ambayo inafanya kazi kwa namna ileile ya kutibu ugonjwa ama tatizo la kiafya. Yapo makundi 5 ya dawa za VVU.

Kundi kidhibiti: Katika majaribio mengi ya kitabibu yenye ulinganifu, kundi moja la washiriki hupata dawa za majaribio wakati kundi jingine linapata matibabu ya tiba ya kiwango. Kiwango inamaanisha ile dawa ambayo kwa kawaida wanapatiwa washiriki ambao hawamo katika lile jaribio la kitabibu kama tiba ya matatizo ya kiafya yanayofanyiwa jaribio. Lile kundi la washiriki wanaopatiwa tiba ya kiwango hujulikana kama kundi kidhibiti.

Kundi la Kipooza-uongo: Kundi la washiriki wa jaribio la kitabibu lililoangukia katika kupokea Kipooza-uongo badala ya ile dawa ya majaribio.

Kundi la kusaidiana: Ni kundi la watu ambao hukutana ili kujadili mambo binafsi yanayohusiana na hali inayowakabili, kwa lengo la kuleta msaada wa kiakili na kijamii (msaada)

Kundi la tafiti za kitabibu kwa watu wazima: Mtandao unaofadhiliwa na Marekani unaojikita katika kupunguza maradhi na vifo miongoni mwa watu wazima walioambukizwa VVU.

Kundi la Uchunguzi: Ni kundi la washiriki wanaotumia dawa ile ya inayofanyiwa jaribio; kinyume na lile kundi la kipooza-uongo

Kundi la uchunguzi: Ni lile kundi la washiriki wanaopewa ile dawa inayofanyiwa

Kupumzika dawa: (Tazama mtiririko wa kukatisha tiba): Kipindi ambacho mtu anayetumia dawa za kupunguza makali ya VVU anapositisha matumizi kwa kwa muda fulani, chini ya usimamizi wa kitiba

Kusajili: Kuandikisha au kumweka mtu katika orodha, kama vile katika jaribio la kitabibu

Kusajili: Kuingizwa katika utafiti wa kitabibu kama mshiriki.

Kushikilia (Retain): Kumzuia mtu ili kumfanya aendelee kuwa mwanachama wa kikundi.

Kushindikana kwa Tiba: Kushindikana kwa dawa ya tiba dhidi ya VVU katika kuzia uambukizo wa VVU.

Kushindwa kitabibu: Tokeo la ama kushindwa ama kurudia-rudia kwa magonjwa yanayohusiana na VVU au kuzorota kwa afya ya mwili ijapokuwa kuna matumizi ya dawa dhidi ya VVU. Kushindwa kitabibu inaweza kutokea kwa sababu ya kushindwa kwa kingamaradhi au muundo wa ongezeko virusi. (Tazama kushindwa kwa kingamaradhi au muundo wa ongezeko la virusi.)

Kushindwa kwa mfumo wa Kinga (Immunologic failure): Kipindi ambapo wingi wa chembechembe za CD4 za mtu mwenye zinashuka chini ya wingi wa kiwango cha msingi, au hakiongezeki zaidi ya wingi wa kiwango cha msingi hata kama anatumia tiba dhidi ya VVU

Kushindwa kwa Virologic (Virologic failure - (Tazama kushindwa kwa Tiba): Kushindikana kwa dawa ya tiba dhidi ya VVU katika kupunguza wingi wa VVU au kuhimili kutoongezeka kwa wingi wa VVU.

Kutozingatia/Bila ufuasi (Non-adherence): Kushindwa au mtu kutokuwa na uwezo wa kutumia dawa kama alivyoelekezwa.

Kuweka mkakati: Kuweka katika vikundi kufuata misingi ya viashiria mahususi vya afya (kama vile idadi ya chembechembe za CD4)

Kuzuia uambukizo wa VVU kutoka kwa Mama-kwenda kwa-mtoto(PMTCT): Ni afua za kuzuia kupeleka VVU kutoka kwa mama mwenye uambukizo wa VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa ujauzito, uchungu na kujifungua, au kunyonyesha ziwa la mama.

L

Lengo: Kitu Fulani ambacho mtu au kundi linataka kufikia; kusudi

M

Maambukizi ya aina ya mlalo: Uambukizo kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine, isipokuwa kwenye kisa cha kutoka-kwa-mama-kwenda-kwa- mtoto (pia inajulikana kama uambukizo wa mlalo)

Maelezo ya Utume: Ni waraka unaoelezea lengo la kikundi, wakala, au shirika.

Majaribio tarajiwa: Hii ni aina ya jaribio linalolenga mbele ya muda wa sasa. Kwa mfano, mtafiti anachagua kundi Fulani la washiriki na kufuatilia matokeo ya matibabu yao kwa kipindi cha miezi 6.

Majaribio ya Baada ya – dawa kuingia kwenye soko (Post-marketing studies) (Angalia Awamu ya IV ya jaribio): Majaribio yanayoendeshwa baada ya dawa mpya kupitishwa na zinatumika.

Majaribio ya kuzuia: Majaribio ya kitabibu za kugundua njia nzuri zaidi ya kuzuia ugonjwa (kama vile VVU) miongoni mwa watu ambao hawapatwa na ugonjwa huo. Njia hizo zinaweza kujumuisha madawa, chanjo, au badiliko la tabia

Malengo ya jaribio (Tazama malengo): Madhumuni ya jaribio la kitabibu

Malengo: Malengo yanayopimika

Manufaa: jambo jema, chanya au ya matokeo mazuri

Manufaa: Ya manufaa. Kuwa na manufaa chanya katika hali Fulani ama ugonjwa

Mapitio ya Wenza (Peer review): Rejea ya jaribio la kitabibu inalofanywa na wataalamu ambao hawahusiki na jaribio hilo. Wataalamu hawa hulipitia jaribio kwa ajili ya kuangalia ufanisi wa kisayansi, usalama wa mshiriki, na mambo mengine ya kimaadili.

Matukio: Matukio ya VVU ni kiwango cha jinsi visa vipya vya VVU vinavyotokea katika idadi ya watu kwa kipindi fulani maalumu. Kwa mfano, matukio ya VVU katika nchi X yalikuwa 500/100,000 kwa mwaka.

Matumizi ya huruma: Istilahi inayotumika kuelezea programu yoyote inayotoa dawa nje ya majaribio ya kitabibu kwa wagonjwa ambao hawana tiba ya uchaguzi.

Matunzo ya-kinifu ya kiafya: Kutoa huduma ya matunzo yakiongozwa na matokeo ya utafiti wa kitabibu.

Mdau: Ni mtu au kundi lililo na shauku ya moja kwa moja au kujuhusisha katika kitu fulani

Meneja wa takwimu: Mtu ambaye amebobea katika kupanga na kuhifadhi takwimu zilizokusanywa wakati wa majaribio ya kitabibu

Mfadhili: Shirika, Wakala, au kikundi kinachotoa fedha kwa ajili ya jaribio

Mikrobisaidi: Ni kitu kinachotumika kwenye ngozi au utando (Kama vile katika uke) ili kuua virusi ama bakteria. Kwa kuhusiana na VVU, mikrobisaidi ya mafanikio ingekuwa ile ambayo ingepunguza hatari ya uambukizo wa VVU kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine wakati wa kujamiiana.

Mkondo mmoja: Tiba au kundi la kipooza-uongo katika majaribio ya tabibu yanaweza kuelezewa kama mkondo wa tafiti/jaribio hilo.

Mkusanyiko wa Kanuni za Nuremberg (Nuremberg code): Ni hati inayotumika kimataifa kuongoza yale maadili ya kuendesha tafiti za kitabibu.

Mlipuko: Elimu ya mlipuko kujua lini, wapi, kwa nini, na ni vipi ugonjwa umetokea katika idadi ya watu.

Mnasihi: Ni mtu anayeaminiwa au kiongozi

Mpangilio wa kusitisha dawa (Structured treatment interruption - STI) (Angalia kupumzika dawa.): Ni namna iliyopangwa, ya usitishaji wa matumizi ya dawa dhidi ya VVU, chini ya uangalizi wa madaktari kwa kipindi cha muda maalumu.

Mpangilio wa tathmini (pia hujulikana kama mpangilio wa matukio): Ni mpangilio unaohitajika wa mshiriki kipindi cha jaribio la kitabibu. Inajumuisha vipindi vya kufika kiliniki, vipimo halisia vya mwilini, damu, na vipimo vingine ili kufuatilia hali ya afya.

Mpango wa Jaribio: Ni aina ya afua za kiuchunguzi zinazotumika katika protokali za jaribio la kitabibu. Inajumuisha maelezo kama vile ya uchunguzi, iliyofumbwa - sana, yenye udhibiti wa kipooza-uongo, isiyofuata mpangilio mahususi.

Mratibu wa Jaribio: Ni mjumbe wa timu ya utafiti katika CTU, anayewajibika kwa utawala wa washiriki wa siku-hadi-siku, kukusanya takwimu na kuziweka katika kumbukumbu, kuandaa programu za uhakiki wa ubora, kuwasiliana na IRB au kamati ya maadili, na kutoa taarifa kwa Msimamizi mkuu (PI).

Mshiriki (pia hujulikana kama mlengwa): Mtu wa kujitolea kujiunga na jaribio la kitabibu.

Mshiriki: Aliyejumuishwa na ama sehemu ya…..

Mshiriki: Ni jina jingine la mtu katika jaribio la kitabibu ambaye athari au mafanikio ya tiba hufanyiwa uchunguzi kwake/juu yake.

Msimamizi wa eneo (Site monitor): Ni mtu anayetathmini kazi ya jaribio la kitabibu katika eneo ili kuhakiki sheria zinazohusu utaratibu wa maadili mema, taratibu za kiwango cha utekelezaji, kanuni (za kisheria) na mahitaji ya kufuatwa.

Mtaalamu wa majaribio ya utafiti (CTS): Mtu aliyepo katika kituo cha utabibu wa majaribio ambaye huratibu maendeleo ya protokali,ikijumuisha mawasiliano yote na kuunganisha timu ya utafiti, wafadhili, na mawakala wa taratibu za utafiti

Mtafiti mkuu (PI): Ni yule mtafiti kiongozi wa jaribio maalumu la kitabibu au mtafiti mkuu ambaye ni msimamizi wa tafiti zote zilizopo katika kituo cha tafiti za kitabibu.

Mtafiti: Mtafiti

Mtafiti: Mwana sayansi anayesaidia kuandaa, kuhimili/kumeneji, na kuchambua matokeo ya jaribio hilo la kitabibu

Mtakwimu: Ni mtaalamu wa kisayansi anayehusika na kuchambua takwimu zote zilizokusanywa katika jaribio la utabibu ili

kupata matokeo ya jaribio. Watakwimu ni sehemu ya timu ya protokali, na ni muhimu katika kuandaa majaribio ya kitabibu. Watakwimu huhakikisha kwamba mpango wa jaribio ni muafaka ili kuweza kujibu suali la utafiti linalofanyiwa majaribio.

Mtandao (Angalia mitandao ya tafiti za kitabibu): Kundi la hospitali na kliniki katika maeneo tofauti-tofauti ambazo hushirikiana kuandaa na kutekeleza tafiti za kitabibu zinazohusiana na tatizo maalumu la kiafya. Washiriki kutoka maeneo tofauti-tofauti wanaweza kuingia katika jaribio hilo moja, na washiriki na watafiti kutoka maeneo mengi tofauti-tofauti wanaweza kufanya kazi pamoja ili kuendeleza msukumo wa taarifa na kuboresha huduma ya afya.

Mtandao wa majaribio ya chanjo za VVU (HIV Vaccine Trials Network -HVTN): Ni majaribio ya kitabibu yanayoandaliwa na DAIDS na kujaribisha chanjo za kuzuia ama kutibu VVU

Mtandao wa majaribio ya ki-Mikrobisaidi (MTN): Ni mtandao wa kiutafiti unaofadhiliwa na Marekani wenye kusudio la kuandaa mikrobisaidi za kupunguza uambukizo wa VVU kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine.

Mtandao wa Majaribio ya Kuzuia (HIV Prevention Trials Network) (HPTN): Ni mtandao wa majaribio ya kitabibu unalofadhiliwa na DAIDS ambao huandaa na kujaribu usalama na manufaa ya njia ambazo zisizo za chanjo ili kuzuia kuenea kwa VVU kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine.

Mtandao wa Utafiti wa kitabibu (CTN): Kundi la hospitali na kliliki katika maeneo mbalimbali ambayo hushirikiana katika kuandaa na kuendesha jaribio la kitabibu zinazohusiana na kuzuia ama tatizo maalumu la kiafya. Washiriki kutoka maeneo mbalimbali wanaweza kuingia katika jaribio hilo moja la kitabibu, na watafiti kutoka maeneo mbalimbali wanaweza kufanya kazi pamoja kupeleka mbele maarifa na kuboresha huduma ya afya.

Mtandao wa utafiti: Angalia Mtandao wa utafiti za kitabibu.

Mtetezi: Mtu anayetetea jambo (Mtetezi wa haki sawa kwa wakina mama) AMA Yule ambaye anaongea kwa niaba ya mtu mwingine (mtetezi wa watu walioambukizwa VVU)

Mtu wa kujitolea: Ni mtu anayekubali kushiriki katika jaribio la kitabibu.

Muda: Urefu wa muda…..

Muundo: Mwonekano wa dawa inayotumiwa, kama vile vidonge, kapsuli, au kimiminika

Muunganishi: Ni mtu anayetumika kama kiungo au kiunganishi kati ya mtu na mtu au kikundi

Mwakilishi wa eneo: Mjumbe wa ile timu ya utafiti yenye wajibu wa kutathmini protokali wakati wa uandaaji ili kunga'mua kama yale mahitaji ya jaribio yataweza kwa kiasi cha kutosha kumudu majaribio ya kitabibu (CTU). Kwa kawaida ni mratibu wa majaribio mwenye uzoefu mkubwa, nesi wa utafiti, mtafiti msaidizi, au meneja wa takwimu kutoka CTU.

Mwelimishaji rika: Mtu anayetoa taarifa na mafunzo kwa mtu mwenye msingi ama tabia inayofanana (mfano, vijana-kwa-vijana au wamama wenye uambukizo wa VVU kwa wamama wenye uambukizo wa VVU)

Mwenza/mrika: Mtu mwenye misingi inayofanana au tabia ya kufanana

Mwingiliano wa dawa-na-dawa: Athari isiyotarajiwa ama kuhitajika wakati dawa moja inapotolewa sambama na dawa nyingine

Mwitikio wa Kinga-mwili (Immune response): Ni mabadiliko ya kinga mwilini kwa "kitu kilichoingia" kama vile kirusi ama bacteria.

Mzigo wa vidonge: Hurejea idadi na mpangilio wa vidonge vinavyotumika kila siku katika tiba mahsusi dhidi ya VVU. Mzigo mkubwa wa vidonge unaweza kupelekea kupungua kwa ufuasi wa tiba kwa sababu ya shida ya kumeza idadi kubwa ya vidonge inavyotakiwa.

N

Nadharia tete (Hypothesis): Ni maelezo yasiyo na uthibitisho ambayo hutumika kama kigezo cha jaribio la kitabibu. Kwa mfano, jaribio la kitabibu linalolinganisha dawa ya kupunguza makali ya VVU (ARV) ya majaribio na dawa ya tiba ya kiwango kwa ajili ya kuzuia uambukizo wa VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT)imewekewa kigezo kwenye kiinimacho kwamba ile dawa ya majaribio itakuwa ya manufaa ama manufaa zaidi kwa kupunguza hatari ya uambukizo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto mchanga.

Namba ya kumtambua mgonjwa (PID): Namba ambayo hupewa mshiriki katika jaribio la kitabibu ili kudumisha usiri (usiri) wa taarifa za mtu Fulani zinazokusanywa wakati wa jaribio (takwimu). Taarifa kuhusu mshiriki huyo hutambulishwa kwa namba, badala na jina.

Ngono isiyo na kinga: Ngono bila matumizi ya kondomu

Ngono salama: Inajumuisha taratibu za kufanya ngono ambazo hupunguza kumweka mtu hatarini kwa ambukizo la VVU au magonjwa mengine yanayoambukizwa kwa njia ya ngono

Non-nucleoside reverse transcriptase inhibitors (NNRTIs): Ni kundi kubwa la dawa dhidi ya VVU. Aina hii ya kiini geuzi cha aina ya transcriptase inahitajika ili VVU viweze kuziambukiza chembechembe za mwili na kutengeneza VVU vingi zaidi. NNRTIs huzuia ile kiini geuzi cha aina ya transcriptase isifanye kazi yake vizuri. Mifano ya NNRTIs ni delavirdine (DLV), efavirenz (EFV), na nevirapine (NVP).

Nucleoside reverse transcriptase inhibitors (NRTIs): Ni kundi kubwa la dawa dhidi ya VVU. Kundi hili la dawa dhidi ya VVU huzuia kuzaliwa kwa VVU vipya kwa namna ile lie inayofanana na NNRTIs, lakini hutumia aina tofauti ya kiini geuzi. Mifano ya NRTIs inajumuisha abacavir (ABC), didanosine (ddI), lamivudine (3TC), stavudine (d4T), zalcitabine (ddC), na zidovudine (ZDV or AZT).

Nucleotide reverse transcriptase inhibitors (NTRTIs): Ni kundi kubwa la dawa dhidi ya VVU yenye asili ya nucleotides, ambazo zimebadilishwa kiini geuzi ili kuzuia ile shughuli ya aina fulani ya protini ambayo ni muhimu kuzalisha VVU. Mifano ya NTRTIs inajumuisha adefovir dipivoxil (ADV) na tenofovir (TDF).

Nyoroo: Kitu kisichofanya kazi

P

Pediatric AIDS Clinical Trials Group (PACTG): Ni Mtandao wa Utafiti wa VVU unaofadhiliwa na DAIDS katika kujifunza juu ya tiba ya VVU ama watoto wenye

uambukizo na vijana na afua za kuzuia uambukizo wa VVU kutoka wa mama-kwenda kwa-mtoto. Mwaka 2006, PACTG ilijiunga na sehemu ya HPTN na kuwa kundi la International Maternal, Pediatric, and Adolescent Clinical Trials (IMPAACT).

Perinatal: Ni kipindi kinachokaribiana na muda ule wa ujauzito, uzazi, na unyonyeshaji.

Pharmacokinetics (PK): Ni jaribio la kugundua kile kiasi cha dawa kilichipo ndani ya damu. Jaribio hili la damu huonesha jinsi dawa inavyonyonywa na kusambazwa ndani ya mwili baada ya kunywewa.

Postnatal: Baada ya kuzaa

Postpartum: Baada ya kuzaa

Prenatal (Angalia Antenatal): Kabla ya kuzaa

Prophylaxis: Ni tiba ya kuzuia ugonjwa maalumu au kuzuia kujirudia kwa ugonjwa uliopo ambapo tayari umekwishawekwa katika hali ya kuzuilika.

Protokali (Mpangilio): Utaratibu ama mpangilio wa jaribio. Huo Utaratibu ama mpangilio wa jaribio umeandaliwa ili kulinda afya ya washiriki na kujibu maswali mahususi ya utafiti. Protokali huelezea ni aina gani ya watu wanaweza kushiriki katika jaribio, utaratibu wa vipimo, taratibu, matibabu, na dozi (kipimo); na muda wa hilo jaribio. Wakiwa ndani ya jaribio hilo la kitabibu, kwa kufuatana na protokali, washiriki wataonwa mara kwa mara na wafanyikazi wa utafiti ili kufuatilia afya zao na kuangalia usalama na ubora wa hiyo tiba.

R

Ridhaa: Mchakato wa kujifunza mambo yote ya kweli kuhusu jaribio la kitabibu kabla ya kuamua kama utashiriki. Mchakato wa ridhaa uanaendelea kipindi chote cha jaribio ili kutoa taarifa kwa washiriki, ambao wengine wanaweza kuamua kusitisha kushiriki katika jaribio wakati wowote.

S

Saikososho (Psychosocial): Inahusiana na ustawi wa kiakili na wa kijamii kwa pamoja

Sampuli: Tazama sampuli.

Shirika la Afya Duniani (World Health Organization - WHO): Ni wakala wa Umoja wa Mataifa ulioanzishwa mwaka 1948 ili kuendeleza ushirikiano wa katika kuboresha hali za afya. Shirika la Afya Duniani lilipewa mamlaka mapana chini ya katiba yake ili kutia msukumo wa kupatikana “kiwango cha juu kabisa cha afya” kwa ajili ya watu wote.

Shirika la Chakula na Dawa (Food and Drug Administration…..FDA): Ni wakala wenye wajibu wa kuhakiki usalama na manufaa ya dawa, chanjo, na vifaa vya kitabibu vilivyopatiwa leseni Marekani

Sio-Salama: Yupo katika hatari ya hisia ya kuumia au madhara ya kimwili; rahisi kurubuniwa au kukubaliana kama akishinikizwa.

Skima: Upangiliaji wa taratibu za protokali, ikijumisha malengo ya jaribio, kupanga makundi bila utaratibu maalumu, idadi ya washiriki, mikondo ya tiba, na vigezo vya kutoa jibu la mafanikio ya tiba au kushindikana kwa tiba.

T

Taasisi ya Kimataifa ya Mzio na Magonjwa Kuambukizwa—(National Institute of Allergy and Infectious Diseases-NIAID): Ni wakala anayefadhiliwa na serikali ya Marekani anayewajibaka kuendesha na kusaidia utafiti kwa ajili ya kuelewa zaidi, kutibu, na kuzuia uambukizo, usugu, na magonjwa ya mzio).

Taasisi ya Kitaifa ya Afya (National Institutes of Health - NIH): Ni Taasisi ya mafunzo ya Serikali ya Marekani ambayo inayofadhiliwa na serikali ya Marekani kwa ajili ya utafiti wa afya. Inaendesha utafiti katika maabara zake yenyewe na kusadia tafiti katika vyuo vikuu, shule za tiba, mahosipitali na taasisi nyingine za utafiti, ndani ya Marekani na maeneo mengine ya kimataifa.

Taasisi ya Kitaifa ya Afya ya Mtoto na Maendeleo ya Binadamu (National Institute of Child Health and Human Development - NICHD): Ni wakala anayefadhiliwa na Serikali ya Marekani mwenye utume wa kuhakikisha kwamba kila mtoto anazaliwa na afya njema na anahitajika, kwamba mwanamke hawapati madhara kutokana na kuzaa watoto, na kwamba watoto wanakuwa na nafasi ya kupata afya njema zaidi na maisha mazuri zaidi yenye tija kadiri inavyowezekana.

Taasisi ya Kitaifa ya Magonjwa ya Akili (National Institute of Mental Health - NIMH): Taasisi ya utafiti wa afya ya akili inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani iliyo na utume wa kupunguza mzigo wa magonjwa ya akili na ya kitabia kupitia utafiti.

Takwimu za awali: Taarifa inayoainishwa kuhusu mshiriki kabla tiba ya jaribio kuanza. Ili kupata tokeo juu ya mafanikio ya tiba, takwimu za msingi zinalinganishwa na takwimu zinayopatikana baadaye katika jaribio hilo.

Takwimu: Taarifa zilizokusanywa wakati wa jaribio la kitabibu

Tamati ya kitabibu: Katika jaribio la kitafiti, tamati ya kitabibu inamaanisha ugonjwa, dalili, ama dalili kwamba mojawapo ya viashiria ndio ama sivyo tiba hiyo ni salama ama ya manufaa. Kwa mfano, jaribio la kitabibu linalododosa uwezo wa dawa kwa ajili ya kuzuia shinikizo la damu linaweza kusababisha maumivu ya kifua kama tamati ya tiba hiyo.

Tamati/ukomo: Badiliko lililothibitishwa juu ya mtu aliyepo katika jaribio la kitabibu linalotumika kuainisha kama huduma ni ya manufaa. (Tazama Tamati ya kitabibu) Tamati ya maabara ianamaanisha kitu ambacho chaweza kupimika kwa kutumia kipimo kingine cha damu (kama vile kipimo cha wingi ama uchache) au kipimo kingine cha upimaji wa maabara.

Taratibu Muafaka za jaribio (GCP): Seti yenye viwango vya miongozo (taratibu na sheria) kwa ajili ya kuandaa; kutekeleza; kufuatilia; kuweka kumbukumbu, kuchambua, na kutoa taarifa ya matokeo ya tafiti za kitabibu

Taratibu za Kisayansi na Kijamii (Social and Scientific Systems-SSS): Makazi ya 'the Operations Center kwa ajili ya IMPAACT na kundi la Adult AIDS Clinical Trials.

Taratibu za Kiwango cha utendaji (Standard operating procedure -SOP): Hati zilizoandikwa zinazoelezea kwa kina jinsi gani utendaji unatakiwa kufuatwa.

Tathmini: Majaribio au uchunguzi unaofanyika wakati wote wa jaribio la kitabibu ili kuhakiki hali ya kiafya ya washiriki

Teratogenic: Inaleta madhara kwa kiumbe tumboni kwa kuingilia ukuuaji wa kawaida katika mimba.

Thibitisho: Kuthibitisha au toa kwa uhakika.

Tiba (Tazama tiba ya kiwango.): Ni mpangilio wa tiba ambao wataalamu hukubaliana kwamba ni sahihi, uliokubalika, na unatumika kwa wingi kwa ajili ya ugonjwa au hali fulani

Tiba baada ya hatari ya uambukizo wa VVU (Post-exposure prophylaxis-PEP): Ni tiba ya VVU inayotolewa kusaidia kuzuia maambukizi baada ya hali juu ya hatari ya uambukizo wa VVU (kama vile kuumia kutokana na sindano zisizo salama, ama kubakwa)

Tiba isiyohitaji akiba ya Protease (Protease-sparing regimen): Ni aina ya dawa dhidi ya VVU ambayo haijumuishi dawa inayotokana na kundi la kizuizi cha aina ya protease.

Tiba ya daraja la pili (Second-line treatment): Ni tiba ya dawa za kupunguza makali ya VVU(ARV) zinazotolewa kwa watu waliojenga usugu kwa ile tiba ya daraja la kwanza la dawa za kupunguza makali ya VVU, au walioshindikana kwa tiba.

Tiba ya dawa za kupunguza makali ya VVU (ART): Ni mfumo wa kutibu kwa kutumia madawa dhidi ya VVU au dawa.

Tiba ya kanuni ya mwanzo (Tazama Tiba-kanuni ya mwanzo): Kundi la kwanza la dawa za kupunguza makali ya VVU (ARV) na hutumika katika kutibu VVU kwa kila mtu.

Tiba ya kiwango (Tazama Tiba ya matunzo.): Tiba kwa ajili ya ugonjwa au hali ambayo mtu angepatiwa iwapo hakusajiliwa katika jaribio la kitabibu. Tiba iliyoidhinishwa.

Tiba ya kuimarisha kinga (Immunotherapy—also known as immune-based therapy or IBT): Tiba ya kusisimua ama kuimarisha mfumo wa kinga ya mwili kupigana na maradhi.

Tiba ya kunusuru(Salvage therapy): Tiba dhidi ya VVU kwa watu ambao wamekwisha kutumia aina mbalimbali za dawa dhidi ya VVU katika kipindi cha nyuma, wamekwisha kushindwa angalau aina mbili za tiba dhidi ya VVU, na wanao usugu mwingi kwa dawa dhidi ya VVU.

Tiba ya uchunguzi: Ni jaribio linalochunguza tiba mpya ama mchanganyiko wa dawa

Timu ya Jaribio: Mtafiti mkuu pamoja na wataalamu wengine (kama mwakilishi wa jamii) na wafanyakazi wanaoendesha jaribio la kitabibu

Tokeo hasi la haraka (EAE): Tukio lolote la matokeo hasi ambalo ni lazima taarifa zake zitolewe haraka kwa DAIDS kama ilivyoainishwa na hiyo protokali

U

Uambukizo toka kwa mama-kwenda kwa-mtoto (MTCT): Uambukizo wa VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa ujauzito, uchungu na kujifungua, ama kwenye unyonyeshaji. Pia hujulikana kama uambukizo wa wima.

Uambukizo toka kwa wazazi-kwenda kwa-mtoto (PMTCT): Ni msamiati unaopendelewa kutumika katika nchi kadhaa (kunyume na MTCT, au uambukizo kutoka kwa mama-kwenda kwa-mtoto) kwa sababu inaweka wajibu kwa ustawi wa huyo mtoto kwa wazazi wote, badala ya kwa mama peke yake.

Uambukizo wa aina ya wima (Vertical transmission): Uambukizo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto mchanga wakati wa ujauzito, uchungu na kujifungua, ama kunyonyesha ziwa la mama

Uambukizo wa msingi: (Pia najulukana kama uambukizo mpya). Ni kipindi ambacho VVU huzaliana haraka (kuongezeka idadi ya VVU ndani ya mwili) ambacho hutokea muda mfupi baada tu ya kupata uambulizo wa VVU.

Uandikaji wa hati ya Mwanzo/ Awali (Source documentation): Ni ushahidi ulioandikwa ambao takwimu zake zimetolewa taarifa katika jaribio la kitabibu na ni za sahihi na za kweli. Kwa mfano, taarifa ya kutoka maabara inaweza kutumika kama hati ya Mwanzo ikionesha kwamba kipimo cha wingi wa virologia ulifanyika kwa mshiriki tarehe hiyo iliyotolewa taarifa, na kwamba majibu yanafanana na yale yanayotolewa taarifa kwa ajili ya jaribio.

Ubaguzi: Kumtendea mtu au kundi isivyo haki au sawa kwa misingi ya dhuluma

Uchambuzi wa Takwimu: Kuzitafakari Taarifa zilizokusanywa wakati wa jaribio la kitabibu ili kutambua matokeo ya hilo jaribio

Uchanganyaji: Utaratibu wa ujazaji wa vimiminika katika mishipa aina ya veni.

Uchunguzi wa ki-historia ya asili ya kitu: Uchunguzi wa maendeleo ya asili (mwendelezo) wa ugonjwa kwa kipindi fulani. Hili neno “asili” linamaanisha kwamba hakuna afua ya kuzuia au kusimamisha ugonjwa inayotolewa wakati wa uchunguzi. Uchunguzi wa ki-historia ya asili ya ugonjwa wa VVU haifuati maadili tena kwa sababu tiba ya VVU ipo. (Majaribio ya kitabibu ya VVU ni lazima yajumuishe tiba dhidi ya VVU wakati tiba inapohitajika.)

Uchunguzi wa kitabibu: Utafiti unaohusisha watu (Tazama Utafiti wa Kitabibu)

Ufuasi: Kutumia kipimo sahihi cha dawa na kwa wakati muafaka

Ufuatiliaji: Kitendo cha ziada kinachotokana…..; na kinachodhamiria kuongeza kitu cha ziada kwa kitu kilichokwisha kufanyika awali

Ugonjwa nyemelezi (OI): Ni ujonjwa unaosababishwa na vimelea vya aina nyingi, miongoni mwao ni vile ambavyo kwa kawaida havisababishi magonjwa kwa watu ambao kingamwili zao ni imara. Watu wanaoishi na VVU katika hatua iliyosogea wana kingamwili iliyoharibika, hivyo kuweka mianya ya kujipenyeza maradhi ambayo yangeweza kuzuilika.

Ugonjwa: Maradhi

Uhakiki wa ubora (thamani)—(Quality assurance - QA): Ni ule mpangilio wa matukio yaliyoandaliwa ili kuhakikisha kwamba jaribio la kitabibu linaendeshwa kwa kufuatana na makubaliano na Miongozo Mizuri ya Utendaji ya Kitabibu na taratibu zake (kisheria).

Uhamasishaji: Desturi ya kuchukua hatua ya moja kwa moja kuunga kono ama kupinga hoja ama sababisho Fulani.

Ukiukwaji wa maadili ya kisayansi: Wakati mtafiti anapokiuka sheria, maadili ya utafiti. Kwa mfano: kusema uongo, kugushi takwimu, kuiba kazi za watafiti wengine.

Umadhubuti wa takwimu: Ni uwezekano wa ile tofauti katika matokeo kati ya kundi la uchunguzi na lile la tiba ya kiwango iliyotokea kwa sababu ya tiba au ile afua badala ya kubahatisha peke yake. Katika jaribio la kitabibu, kiwango cha umadhubuti wa takwimu unategemeana na idadi ya

washiriki waliofanyiwa uchunguzi na mambo yaliyoangaliwa, na pia ukubwa wa hiyo tofauti iliyoonekana.

Unasihi na upimaji wa hiari (VCT): Inahusiana na kumnasihi mtu kuhusu VVU kabla ya kusihi ridhaa yake kufanya kipimo cha kinga-maradhi ya VVU.

Unasihi: Majadiliano ya siri kati ya mtu mmoja na mtoa huduma wa afya

Unyanyapaa: Ni alama au tendo la kufadhaisha.

Unyonyeshaji-pekee: Kutoa virutubisho kwa mtoto mchanga kwa ziwa la mama tu (hakuna maji, maziwa ya kopo, au chanzo kingine chochote cha virutubisho kinachotolewa).

Upanuzi wa ziada: Mpango wa majaribio ya dawa unaotolewa kwa watu ambao hawakufikia kiwango cha kuingia katika jaribio la kitabibu

Upendeleo usiostahili: Maamuzi yasiyo ya haki. Wazo ambalo linafungamana badala ya kutofungamana

Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI): Hatua ya mwisho na kali zaidi ya ugonjwa kutokana na uambukizo wa Virusi Vya UKIMWI (VVU.

Usalama: Kuweka ukingo wa madhara hatarishi yanayotarajiwa kutokana na tiba

Ushirikiano: Kufanya kazi pamoja kwa lengo moja la pamoja.

Usimamizi: Kuangalia, kufuatilia kwa karibu, au kuhakiki (mara nyingi kwa madhumuni mahususi) 1) Washiriki wa utafiti za kitabibu hufuatiliwa kwa karibu kuona matokeo kinzani ya tiba. 2) Vitengo vya Tafiti za kitabibu kufuatuliwa na wataalamu wa nje ili kuhakikisha kwamba utafiti unaendeshwa kufuatana na Miongozo ya maadili sahihi na kwa kufuatana na sheria za serikali zilizopo.

Usiri: Kuficha taarifa binafsi. Taarifa binafsi zilizokusanywa wakati wa majaribio ya kitibabu haziwekwi katika kumbukumbu ama kutolewa kwa kutumia jina, tarehe ya kuzaliwa, au aina nyingine zozote za taarifa binafsi.

Ustahimilivu: Kuonesha ni kwa namna gani bora watu wanaweza kustahimili kwa aina fulani ya dawa wanapozitumia katika dozi ya kawaida. Ustahimilivu mzuri unamaanisha kwamba athari mbaya hazisababishi watu kusita kuzitumia hizo dawa.

Usugu wa dawa: Uwezo wa kirusi kama VVU (ama bakteria) kubadilika ili kuendelea kuzaana, hata kama kuna matumizi ya dawa ambayo kwa kawaida inamuua

Usugu wa iana nyingi za dawa (MDR): Uambukizo (kama vile VVU) ambao hubadilika ki-tabia au maumbile kutoka hali yake ya asili na kuwa haitibiki na dawa ambazo hapo awali zilikuwa zinatibu kikamilifu.

Usugu: Hutokea wakati VVU vimebadilika na kuwa sugu (kubadilika) kwa jinsi ambayo kinapata uwezo wa kuishi na kuzaliana licha ya kuwepo dawa dhidi ya VVU. Kwa nyongeza, usugu huu hukitengenezea kirusi uwezo wa kuishi na kuzaliana katika mazingira ya dawa zinazofanana na hizo za kudhibiti VVU. Kwa mfano, usugu wa dawa moja kwenye kundi, m.f. ya NNRTI, kwa kawaida huzalisha usugu kwa dawa zote katika daraja hilo, kwa hiyo, usugu kwa dawa zote za aina ya NNRTI.

Usugu: Ni neno linalotumika kuelezea uwezo wa VVU kubadilisha umbile lake ili kuifanya dawa dhidi ya VVU (ARV) isiwe ya manufaa. Kujijenga kwa usugu huu kwa

aina moja ya dawa dhidi ya VVU (ARV) mara nyingi ina maanisha inaleta usugu kwa dawa zote za kupunguza makali ya VVU ndani ya kundi hilo la dawa. Usugu unaweza kujijenga kama tokeo la kushindikana kwa ufuasi wa dawa iliyotolewa.

Utabiri: Ni dalili ya kuashiria kuleta nafuu(au bila kuleta nafuu) katika misingi ya kawaida ya ugonjwa na/au uwezekano kwamba tiba ya ugonjwa huo itakuwa ya manufaa.

Utafiti wa Kitabibu: Utafiti unaohusisha watu. Utafiti unaohusisha watu ni njia ya haraka kuliko zote na salama katika kupata tiba ya manufaa, salama kwa ugonjwa, hali, ama dalili.

Ute wa uti wa mgongo (CSF): Ni vimuminika vinavyoogelea kwenye uti wa mgongo na ubongo. Sehemu ya vimiminika hivyo vyaweza kutolewa kwa matumizi ya mafunzo kwenye maabara, kwa mfano, kupima idadi ya VVU katika CSF, ama kuthibitisha dalili za uambukizo ndani ya vimiminika hivyo.

Uwazi: Kumjulisha mtu mwingine au watu wengine kuhusu hali ya uambukizo wa VVU

Uwezo wa kuleta-Sumu: Uwezo wa kuweka sumu ama kuathiri vibaya mwili

Uzoefu wa -Tiba: Watu wenye uambukizo wa VVU ambao kwa wakati huu wapo katika tiba dhidi ya VVU au wamekwesha kutumia dawa katika kipindi cha nyuma.

V

Virologisti: Ni mwanasayansi, kwa kawaida ni daktari wa tiba, ambaye amekubuhu katika utaalamu wa virusi.

Vizuizi mwingiliano: Kundi la dawa dhidi ya VVU zinazozuia kuingiliana (kukaa pamoja) kwa lile ganda la nje la VVU na chembechembe ya CD4, na hivyo kuzuia VVU visiathiri chembechembe ya CD4 (au chembechembe ya T).

Vizuizi vya aina ya kiini cha Integrase: Kundi la dawa dhidi ya VVU ambayo huzuia protini aina ya integrase kuweka taarifa za VVU kwenye chembechembe za VVU katika DNA (mfumo wa kuunda chembechembe hai, jenasi) ya chembechembe ya CD4 ambayo ina uambukizo

VVU: Virusi Vya UKIMWI: Kirusi kinachosababisha uambukizo na UKIMWI

VVU-1: Ni aina ya kirusi kinachojulikana zaidi

VVU-2: Ni aina nyingine ya VVU ambavyo si vya kawaida kama VVU-1. Vinapatikana hasa Afrika ya Magharibi na ina mwenendo wa taratibu zaidi,na vina madhara ya kiasi kidogo ya kitabibu.

W

Wadau wa Jamii: Kamati inayoundwa kusukuma mbele ushiriki wa manufaa na mawasiliano miongoni mwa jamii nyingi na wa muda muafaka, huko Marekani na kimataifa, ndani ya maeneo ambamo mtandao wa tafiti za kitabibu zinazofadhiliwa na DAIDS.

Wawili wanaohusiana bila kufanana: Jozi ya washirika wa ngono, ambapo mmoja ana uambukizo wa VVU na huyo mwingine hana

Wazo: Katika muktadha ya dodoso kwa ajili ya jaribio la kitabibu, wazo ni maelezo ya kifupi ya dodoso hilo la jaribio.

Wenza: Kundi la washiriki katika jaribio la kitabibu ambao wamejumuishwa kufuatana na kigezo cha kufanana(mfano uzoefu wao wa awali wa dawa za kupunguza makali ya VVU-ART)

Western blot (WB): Kipimo cha ki-maabara kwa ajili ya aina maalumu ya kinga-maradhi, ambacho hutumika kuthibitisha kuwepo majibu ya uambukizo wa VVU zaidi ya vipimo vya ELISA or EIA.

Wild-type virus: Aina ya Virusi ambavyo bado havijapata mabadiliko ya ki-jenetiki ambazo hutengeneza tabia maalumu, kwa mfano usugu kwa aina fulani ya dawa.

Wingi/mzigo wa VVU (VL): Kiasi cha VVU katika damu. Wingi/mzigo wa VVU waweza kuonesha kiwango cha shughuli za VVU, na kuonesha iwapo zile dawa za kupunguza makali wa VVU ni za manufaa. Wingi wa VVU hushushwa na dawa za manufaa za kupunguza makali wa VVU.

Wingi/mzigo wa VVU usioweza-kugundulika/kuonekana (Undetectable viral load): Ni matokeo ya kipimo cha wingi/mzigo wa VVU ambacho huonesha kiasi cha virusi ndani ya sampuli hiyo ya damu kuwa ni kidogo mno kugundulika/kuonekana katika maabara. Wingi wa VVU usioweza-kugundulika kwa kawaida unaonesha kwamba tiba ni ya manufaa na/au mtu huyo yupo katika hatari ndogo sana ya kuendelea kwa ugonjwa wake au kujenga usugu kwa dawa yoyote ya kupunguza makali ya VVU (ARV) anazozitumia.

Y

Ya-mfumo/utaratibu: Ni neno linoalotumika kuelezea ugonjwa au tiba inayoathiri mwili kwa ujumla

Z

Zizuizi aina ya Protease (Protease inhibitors-PIs): Ni kundi kubwa la dawa dhidi ya VVU ambayo huzuia kitendo cha kimeny'enya/kiini aina ya protease, inayohitajika kwa ajili ya kutengeneza VVU zaidi. Mifano ya PIs inajumuisha amprenavir (APV), atazanavir (ATV), indinavir (IDV), lopinavir (LPV), lopinavir/ritonavir (LPV/r), nelfinavir (NFV), saquinavir (SQV) na saquinavir soft-gelatin capsule (SQV-sgc).

Vifupisho

Vinavyotumika kwa kawaida katika tafiti za kitabibu

A

ACTG: AIDS Clinical Trials Group—Kundi la Jaribio la Kitabibu la UKIMWI

ABC: abacavir

ABCs: of HIV prevention: abstinence, be faithful, condoms—Ya kinga ya VVU—kuacha kabisa, Kuwa mwaminifu, kutumia kondomu

ACTU: AIDS Clinical Trials Unit—Eneo la Jaribio la kitabibu la UKIMWI

ADAP: AIDS Drug Assistance Program (state programs in US)—Programu ya Msaada ya UKIMWI (Programu nchini Marekani)

ADL: activities of daily living—Shughuli za kila siku za kujikimu

ADV: adefovir dipivoxil

AE: adverse event—Matokeo hasi

AER: adverse event reporting—Kutolea taarifa matokeo hasi

AETC: AIDS Education and Training Center—Kituo cha Elimu na Mafunzo ya UKIMWI

AIDS: acquired immunodeficiency syndrome—Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI au Dalili zinazopatikana zinazopunguza kingamwili)

APV: amprenavir

ART: antiretroviral therapy (or antiretroviral treatment)—Huduma ya dawa za kupunguza makali ya VVU (au tiba ya kupunguza makali ya VVU)

ARV: antiretroviral—dawa za kupunguza makali ya VVU

ATN: Adolescent Treatment Network—Mtandao wa Tiba kwa Vijana

ATV: atazanavir

AZT: zidovudine, ZDV

B

BID: twice daily—Mara mbili kwa siku

BMI: body mass index—kipimo cha ukubwa wa mwili

BSA: body surface area—eneo mraba la mwili

C

CAB: Community advisory board—Bodi ya Ushauri ya Jamii

CBC: complete blood count—Jumla ya wingi wa damu

CBO: community-based organization—Asasi ya Kijamii

CCWG: Cross-CAB working group—Kungi-pitana linalifanya kazi na CAB

CDC: Centers for Disease Control and Prevention—Ni kituo cha Kuthibiti na Kuzuia Magonjwa

CMV: cytomegalovirus

CMI: cell-mediated immunity

CNS: central nervous system—Utaratibu mkuu wa mishipa ya fahamu

CORE: Coordinating and Operations Center—Kituo cha Kuratibu na Utendaji

CPCRA: Community Programs for Clinical Research on AIDS—Programu ya Jamii kwa ajili ya Utafiti wa Kitabibu

CRF: case report form-Fomu ya Ripoti ya Kisa

CS: concept sheet—Fomu ya Wazo/fumbo/fikra

CSF: cerebrospinal fluid—Ute wa kati wa mishipa na uti wa mgongo

CSMB: Clinical Site Management Branch—Tawi la usimamamizi la Eneo la kitabibu

CSMG: Clinical Site Monitoring Group—Kundi la Ufuatiliaji wa eneo la Kitabibu

CT: computed tomography

CTS: clinical trials specialist—Mtaalamu wa Majaribio ya kitabibu

CTU: clinical trials unit—Eneo/Kituo la Jaribio la kitabibu

D

d4T: stavudine

d4T-XR: d4T extended-release capsules

DACS: data analysis concept sheet—Fomu ya Uchambuzi wa Takwimu za Wazo/fumbo/fikra

DAIDS: Division of Acquired Immunodeficiency Syndrome—Idara ya UPungufu wa Kinga Mwilini

ddC: dideoxycytidine (zalcitabine)

ddI: 2í2-dideoxyinosine (didanosine,)

DEXA: dual-energy x-ray absorptiometry

DLV: delavirdine

DMC: Data Management Center—Kituo cha Kusimamia Takwimu

DNA: deoxyribonucleic acid

DOT: directly observed therapy----Tiba ya Kuwa chini ya Uangalizi

DSMB: Data Safety and Monitoring Board—Bodi ya Ufuatiliaji na Usalama waTakwimu

E

EAE: expedited adverse event—matokeo hasi yanayotarajiwa

EBV: Epstein Barr Virus

EFV: efavirenz

EKG (or ECG): electrocardiogram

ENF: enfuvirtide (T-20)

F

FDA: Food and Drug Administration—Uongozi wa Utumiaji wa chakula na dawa

FDC: Fixed-dose combination—Mchanganyiko maalumu wa Dozi

FSTRF: Frontier Science and Technology Research Foundation

FTC: emtricitabine

F/U: follow-up—Kufuatilia

FXBC: FranÁois-Xavier Bagnoud Center

G

GART: Genotypic Antiretroviral Resistance Test

GCP: Good Clinical Practice—Maadili mema ya kufuatwa

GCRC: General Clinical Research Center—Kituo cha Ki-ujumla cha Jaribio la Kitabibu

GLP: Good Laboratory Practice—Utendaji mzuri wa Maabara

GI: Gastrointestinal

GYN: gynecology—Utaalamu wa magonjwa ya wanawake

H

HAART: Highly Active Antiretroviral Therapy—Tiba ya Hali ya Juu sana ya Kupunguza Makali ya VVU

HBV: hepatitis B virus—Virusi vya aina ya hepatitis B

HCV: hepatitis C virus—Virusi vya aina ya hepatitis C

HIV: Human immunodeficiency virus—Virusi Vya UKIMWI (VVU)

HIV RNA-PCR: viral load test (polymerase chain reaction)—Kipimo cha mzigo wa VVU

HPTN: HIV Prevention Trials Network—Mtandao waKuzuia Uambukizo wa VVU

HPV: human papillomavirus

HSV: herpes simplex virus

HVTN: HIV Vaccine Trials Network—Mtandao wa Majaribio ya Chanjo ya VVU

I

IBT: immune-based therapy—Tiba inayolenga Usugu

IC: informed consent—Ridhaa

ICAB: IMPAACT Community Advisory Board—Bodi ya Ushauri ya IMPAACT

ICTU: International Clinical Trials Unit---Kituo cha kimataifa cha Majaribio ya Kitabibu

IDU: injection drug user-Anayejidunga dawa za kulevya katika mishipa(Teja)

IDV: indinivir

IL-2: interleukin-2

IM: intramuscular—Katika misuli

IMPAACT: International Maternal, Pediatric, and Adolescent AIDS Clinical Trials—Mtandao wa Tafiti za Kitabibu za VVU wa Kimataifa kuhusu afya kwa Wanawake, Watoto na Vijana. Investigational new drug—Dawa mpya ya majaribio/uchunguzi

INH: isoniazid

INSIGHT: International Network for Strategic Initiatives in Global HIV Trials—Mtandao wa Kimataifa wa Mikakati katika majaribio ya VVU

IRB: Institutional Review Board—Bodi ya Kitaasisi ya Mapitio

IRD: immune restoration disease—Ugonjwa unaohifadhi usugu

IRIS: immune reconstitution inflammatory syndrome

IRS: immune reconstitution syndrome

K

KPS: Karnofsky Performance Scale

KS: Kaposiís sarcoma

L

L&D: labor and delivery-—Uchungu na Uzazi

LDMS: Laboratory Data Management System—Utaratibu wa Kuhifadhi Takwimu za Maabara

LFT: liver function test-Kipimo cha kuangalia utendaji wa ini

LFU: lost to follow-up—Haweze kufuatiliwa

LIP: lymphoid interstitial pneumonitis

LP: lumbar puncture

LPV: lopinavir

LPV/r: lopinavir/ritonavir, LPV/RTV co-formulation

LSC: laboratory steering committee—Kamati ya uendeshaji ya Maabara

M

MAC: mycobacterium avium complex

MDR: multi-drug resistant—Iliyo na usugu kwadawa nyingi

MAI: mycobacterium avium intracellular

MDR-TB: multiple-drug resistant tuberculosis—TB yenye usugu wa dawa nyingi

MEMS: Medication Event Monitoring System—Utaratibu wa ufuatiliaji Wa matokeo ya dawa

MO: medical officer—Afisa tabibu

MPC: managing partners group—Kundi la usimamizi la Wabia

MRI: magnetic resonance imaging

MTCT: mother-to-child transmission—Kutoka kwa mama-kwenda kwa-mtoto

MTN: Microbicide Treatment Network—Mtandao wa Tiba wa Maikrobisaidi

N

NCI: National Cancer Institute—Taasisi ya Taifa ya Saratani

NEC: Network Executive Committee—Kamati Tendaji ya Mtandao

NFV: nelfinavir

NGO: Non-governmental organization—Asasi zisizo za kiserikali

NIAID: National Institute of Allergy and Infectious Diseases—Taasisi ya Kitaifa ya Mzio na Magonjwa ya Kuambukizwa

NICHD: National Institute of Child Health and Human Development—Taasisi ya Kitaifa ya afya ya Mtoto na Maendeleo ya Binadamu

NIH: National Institutes of Health—Taasisi ya Kitaifa ya Afya

NIMH: National Institute of Mental Health—Taasisi ya Kitaifa Ya Akili

NNRTIs: non-nucleoside reverse transcriptase inhibitors

NRTIs: nucleoside reverse transcriptase inhibitors

NtRTIs: nucleotide reverse transcriptase inhibitors

NVP: nevirapine

NWCS: new work concept sheet—Fomu ya Wazo/fikra ya Kazi mpya

O

OAR: Office of AIDS Research—Ofisi za Utafiti wa UKIMWI

OB: obstetrics

OI: opportunistic infection—Magonjwa nyemelezi

OPS: operations center—Kituo cha Kufanyia kazi

P

PACTG: Pediatric AIDS Clinical Trials Group—Kundi la tafiti za UKIMWI kwa Watoto

PACTU: Pediatric AIDS Clinical Trials Unit—Kituo cha Majaribio ya Kitabibu ya UKIMWI

PCP: Pneumocystis jiroveci pneumonia

PCR: polymerase chain reaction

PEP: post-exposure prophylaxis

PEPFAR: Presidentís Emergency Plan for AIDS Relief—Mpango wa Drarura wa Raisi wa Kuleta Ahueni ya UKIMWI

PERC: performance evaluation resource committee—Kamati ya tathmini ya ufanisi wa nguvu kazi

PGL: persistent generalized lymphadenopathy

PHACS: pediatric HIV/AIDS cohort study

PID: patient identification number (also pelvic inflammatory disease)—Namba ya kitambulisho cha mgonjwa

PI: principal investigator—Mtafiti Mkuu

PI: protease inhibitor—Kizuizi chenye kiini cha protease

PK: pharmacokinetics

PLWA: people living with AIDS—Watu wanaoishi na VVU ama UKIMWI

PML: progressive multifocal leukoencephalopathy

PMPA: tenofovir

PMTCT: prevention of mother-to-child transmission—Kuzuia uambukizo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto

PTCT: parent-to-child transmission—Uambukizo kutoka kwa wazazi kwenda kwa mtoto

PO/po: by mouth; oral route of administration—Kwa njia ya kutumia mdomo.

PP: postpartum (after birth)—Baada ya kujifungua

PPD: purified protein derivative (tuberculin skin test)

PWA: person with AIDS—Mtu mwenye UKIMWI

Q

QA: quality assurance—Uhakiki wa usahihi

QC: quality control—Kutunza ubora

QD: once daily—mara moja kwa siku

QID: four times daily—mara nne kwa siku

QOL: quality of life—thamani ya uhai

R

RAB: Regulatory Affairs Branch—Tawi la kuthibiti ubora wa mambo

RAC: research agenda committee—Kamati ya agenda za utafiti

RBC: red blood cell—chembechembe nyekundu za damu

RCAB: regional community advisory board—Bodi ya ushauri ya Kanda

RCC: Regulatory Compliance Center—Kituo cha kuratibu ulinganifu

RFA: request for applications—Kukaribisha maombi

RFP: request for proposals—uhitaji wa Rasimu

RNA: ribonucleic acid

RT: reverse transcriptase—kimeny'enya aina kigeuzi cha transcriptase

RTIs: reverse transcriptase inhibitors—Kizuizi-geuzi cha aina yenye kiini cha transcriptase

RTV: ritonavir

S

SAE: serious adverse event—Tukio baya hasi

SD: standard deviation—Ukiukwaji wa kiwango

SDAC: Statistical and Data Analysis Center—Kituo cha Takwimu na Uchambuzi wa Takwimu

SGC: soft-gel capsule

SID: study identification number—Namba ya utambulisho ya jaribio

SOC: scientific oversight committee—Kamati ya Kisayansi ya Uangalizi

SOE: schedule of events—Mpangilio wa matukio

SOP: standard operating procedure—Utaratibu wa kiwango cha utendaji

SQV, SQV-sgc: saquinavir, saquinavir soft-gel capsule

SSS: Social & Scientific Systems—Mifumo ya Kijamii na ya Kisayansi

STD: sexually transmitted disease—Ugonjwa unaoambukizwa kwa njia ya kujamiiana

STI: structured treatment interruption (also sexually transmitted infection)—Usitishaji wa dawa kwa mpangilio (pia angalia Ugonjwa unaoambukizwa kwa njia ya kujamiiana)

T

T-20: fusion inhibitor (enfuvirtide)

TB: tuberculosis—Kifua Kikuu

TDF: tenofovir disoproxil fumarate

TID: three times per day—Mara tatu kwa siku

TZ: abacavir/lamivudine/zidovudine co-formulation

U

UDVL: undetectable viral load—Wingi/mzigo wa virusi usioweza Kutambulika/kuonekana

ULN: upper limit of normal—Ukomo wa juu

V

VCT: voluntary counselling and testing—Unasihi na upimaji wa hiari

VL: viral load—Wingi wa Virusi/mzigo wa virusi

VZV: varicella zoster virus

W

WB: Western Blot

WBC: white blood cell—Chembe chembe nyeupe za damu

WHO: World Health Organization—Shirika la Afya Duniani

WNL: within normal limits—iliyo katika kikomo cha kawaida

X

XDR-TB: extreme multi-drug resistant tuberculosis—Usugu mkubwa wa Kifua kikuu kwa dawa za aina nyingi

Z

ZDV: zidovudine (AZT)

Sources:—Vyanzo

- *Clinical Trials Education Series The Basic Workbook* National Cancer Institute (NCI) Cancer Information Service (CIS) May, 2006 http://www.cancer.gov/clinicaltrials/resources/basicworkbook
- *Glossary of HIV/AIDS-Related Terms, 5th Edition*, October 2005. AIDSinfo (A service of the U.S. Department of Health and Human Services). http://www.aidsinfo.nih.gov/Glossary
- Clinical Trials.gov, A Service of the U.S. National Institutes of Health. *Glossary of Clinical Trials Terms.* Developed by the National Library of Medicine, May2006 http://www.clinicaltrials.gov/ct/info/glossary
- *Defining Best Practices for Community Representative Involvement in HIV Clinical Research Networks.* A Cross-CAB Working Group Meeting (Sponsored by the National Institute of Allergy and Infectious Diseases, Division of AIDS. May 6–8, 2005. http://pactg.s-3.com
- *Pediatric AIDS Clinical Trials Group Commonly Used Acronyms.* Pediatric AIDS Clinical Trials Group, October, 2005 http://pactg.s-3.com

- Kwa wale wanaotumia kitini hiki, tafadhali jisikie huru kutuma maoni au maswali kwa: info@fxbcenter.org – Director, IMPAACT International Program FXB Center, UMDNJ 65 Bergen St., GA 36, NJ 07107-1709